

WA KIPEKEE



Na tuombe, Bwana Yesu, tutakapoondoka asubuhi ya leo, tunaweza kusema mioyo yetu iliwaka ndani yetu, kwa kuwa amesema nasi njiani. Tunakushukuru kwa fursa hii nzuri sana ambayo—ambayo imekuwa, ambayo imetujia, tungeweza kukutanika hapa pamoja na watu hawa, watoto Wako, na kufurahia muda huu wa ushirika. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba baraka Zako zitakaa juu yetu tunaposafiri, mahali mbalimbali, na kukutana na wengine.

² Tunakushukuru kwa ajili ya kila ushuhuda wa mazingira haya mazuri ya Kikristo hapa asubuhi ya leo, na kwa ajili ya hawa wote ambao wamekuwa njiani kwa muda mrefu, na kwa ajili ya huyu kijana mwanamume ambaye ndiyo kwanza avuke Yordani, kuona kile inachomaaanisha kweli kuishi. Sote tunaweza kuthamini hilo, Bwana, katika kujua ya kwamba wakati mmoja tulikuwa ule upande mwingine, pia. Bali hakuna tena yale maisha ya kale, sasa. Ni—ni ninii tu . . . Yamerudi Misri.

³ Sasa tunaomba ya kwamba utaubariki ushirika wetu pamoja tunapolisoma Neno Lako, na kuzungumza maneno machache kutoka kwenye hili Neno kuu la Mungu tunaloamini. Na ulibariki kwa mioyo yetu sasa, kuendeleza ibada. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

⁴ Ndugu Leo, Ndugu Gene na wasafiri, ninayahesabu haya kuwa moja ya majaliwa makuu sana ambayo nimekuwa nayo, kuja hapa kujionea mwenyewe kile mliche nacho kwenye maeneo haya. Ni ninii . . . Nimebarikiwa nilipotembea kwenye kijito kidogo pale, na kuona uwanja huu. Nami . . . Wakati mmoja Ndugu Leo alipokuwa akinasa kanda, nami nikamwambia ya kwamba hakika kulikuwako na kitu kikuu zaidi maishani kwa ajili yake zaidi ya kunasa kanda. Na, hakika, kunasa kanda ni jambo ambalo hatuna budi kufanya, bali kumetubariki, lakini kuna kitu kingine. Sote tumeumbwa kwa ajili ya kufanya mambo mbalimbali.

⁵ Na kuja hapa asubuhi ya leo na kuangalia, maskini Yerusalemu hii ndogo hapa nje, ndogo, kile nilichoita, Gosheni, ninaamini, tulipokuja hapa asubuhi ya leo. Kumbukeni, Gosheni ilikuwa ni moja ya mahali ambapo waliabudia, moja ya mahali pa kwanza ambapo hema ilitundikwa. Na kukutana na marafiki wa kale, na—na wapya, na kupewa wakati huu, ninaninii tu . . . Inaonekana kana kwamba—kwamba hutaki kuondoka. Kuna kitu tu kinachotaka kukushikilia. Ninaona ni kwa nini ninyi watu mngetaka kukaa hapa. Mnaona? Ni kitu fulani kinachokushika kwa nguvu.

⁶ Siamini nilipata kuwa katika ushirika na ibada yoyote tamu zaidi, kama nyimbo hizi na kadhalika, ambazo niliketi kule na kuuma midomo yangu na kuitikisa miguu yangu, na kujaribu kujizuia kupiga ukelele, wakati nilipozisikia hizo nyimbo za kale zikiimbwa jinsi ninavyowazia zinapaswa kuimbwa, na ambazo zinaimbwa katika Roho. Sasa, hilo ndilo sisi—sisi... Paulo alisema, “Nikiimba, nitaimba katika Roho.” Sasa, siwezi kuwazia kwamba Roho ni kupiga makelele kwa sauti yetu yote. Na—nafikiri Roho wa Kristo ni upendo, na unyenyekevu, na amani, ambayo—ambayo huleta kitu fulani kwa nafsi zetu, kinachotulisha. Nafikiri, hapo, hivyo ndivyo nyimbo hizo zinavyopaswa kuimbwa.

⁷ Na kuwa hapa pamoja nanyi, watu waliojiweka wakfu kwa huduma, huduma ya Kristo; kuna mambo mengi sana ninge—ningeweza kusema, ambayo wakati usingeniruhusu. Ni—nilikuja kwa ajili... Niliwazia, “Vema, nitakimbia huko na kumtembelea Ndugu Leo na kanisa kule juu na sehemu ya Mwili wa Kristo unaokungojea Ku—Kuja Kwake, na sehemu ya Bibi-arusi aliye hapa ugenini.”

⁸ Na jinsi mmejitenga na ulimwengu mwingine, na—na kuja hapa kuishi jinsi hii. Nilikuwa nikiwazia, hata kile kijito kidogo, mko ng’ambo hii ya Yordani sasa, mko—mko kwenye e—eneo hili hapa. Mme—mmekuja humu kwa kutoka, kutoka ulimwenguni, kuingia mahali ambapo mnaweza kukusanyika pamoja na—na kumwabudu Mungu, kweli kulingana na mwongozo wa dhamira zenu.

⁹ Na hilo ndilo tunalotetea, kama demokrasia, kama taifa. Tunalitetea jambo lili hili, kwamba kila mtu anaweza kuabudu. Na ni vibaya tu sana hatuna mengine kama haya. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ambapo, wanaouacha ulimwengu uwe mahali pao. Na watu wa Mungu wawe mahali pao, ambapo tunaweza kuwa na jambo hili.

¹⁰ Na hakika ninaninii... Kama—kama ningesema “amina” na kutoka mlangoni, ningesema ingenifaidi kuja hapa kwa motokaa kila Jumapili, ama—ama kuwaacha watoto wangu waje hapa, ku—kuketi chini ya mazingira kama haya. Kwa sababu, daima mazingira ndiyo yanayoleta matokeo.

¹¹ Unaweza kuweka mbegu huko ardhini. Haidhuru mbegu hiyo imerutubishwa jinsi gani, na kukaa pale, haina budi kuwa na mazingira fulani ya kuifanya iishi. Mnaona? Jua hilo halina budi kufikia kwenye nguvu fulani, kabla, kuileta katika mazingira fulani. Yai halina budi kuwa na mazingira, la sivyo halitaangulika. Haijalishi ni rutubifu jinsi gani, halina budi kupata mazingira hayo.

¹² Nami nafikiri, kwamba katika kundi kama hili, Wakristo wanaanguliwa, wanazaliwa mara ya pili katika mazingira kama haya. Nilizaliwa chini ya mazingira kama haya. Haidhuru

ninapoenda na kutembelea, ulimwengu baridi, na kwenye huduma za kimishenari na kadhalika, hata ninaweza kusimama na kuyafunga macho yangu na kuwaza juu ya mazingira haya.

¹³ Hii inanikumbusha wakati nilipokuwa mvulana tu mhubiri na nikianza tu. Tulikuwa na makundi madogo yaliyokutana nyumba kwa nyumba. Tulijitenga na mambo ya ulimwengu, pia. Hilo ndilo lililoufanya moyo wangu jinsi ulivyo leo hii, kumpenda Kristo, ambamo tunaweza kukaa pamoja.

¹⁴ Ninaamini Maandiko yalisema, “Ni vizuri jinsi gani kwamba ndugu wanaweza kuishi pamoja katika umoja! Ni kama mafuta ya kupaka yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka kwenye pindo za mavazi yake.”

¹⁵ Na me—mengi tu yangeweza kusemwa. Mimi—mimi... Labda Roho Mtakatifu atawafasiria, nikiisha kuondoka, kwamba ni kitu gani. Laiti ningaliweza kukaa alasiri yote, na kuacha vyakula na chochote kile, niketi tu hapa na kuwasikia mkiimba. Mnaona? Kuwasikia mkiimba, na kuzungumza, na kushuhudia, linamaanisha mengi sana.

¹⁶ Binti yangu anahitimu usiku wa leo. Ama, ni ibada ya kumaliza sekondari, usiku wa leo, nami sina budi kurudi upesi. Nami sikujua hivyo, kwamba ilikuwa ni leo, ambapo ibada ya kuhitimu itafanywa, mpaka jana usiku. Kidogo nina shughuli nyingi, na sikujua hilo.

¹⁷ Na nikiwatembelea pamoja na Ndugu Leo na Ndugu Gene, wanaposhuka kuja hapa, nimetamani kupata wakati wa kuja hapa, nikishangaa, kweli tu. Niliwasikia watu wakisema, “Vema, wana uga wa mkokoteni unaopendeza. Wako kule upande mmoja. Ulimwengu uko upande huo mwingine. Na upande *huu* wote ni maisha yaliyowekwa wakfu na kadhalika.”

¹⁸ Nikawazia, “Ningetaka kuona jambo hilo. Ni—ninataka tu kuona kile kilicho hasa.” Nanyi nyote mmebarikiwa kuwa hapa.

¹⁹ Ni—ninataka kusoma kifungu kimoja tu kutoka kwenye Biblia. Nami ninawazia, kusoma tu kifungu hiki kimoja kutafanya ibada kamili. Lakini ninayo, nikija hapa, nilikuwa na matamshi machache tu ambayo niliwazia ningesema. Haitanichukua ila dakika chache tu. Halafu ningetaka kutoa matamshi haya kwa yale—yale ninayojisikia sasa. Katika Kitabu cha Wakorintho wa Pili, mlango wa 12, na kifungu cha 11, ningetaka kukisoma hiki. Paulo akinena.

Nimekuwa mpumbavu katika kujitukuza, ninyi mmenilazimisha. Maana ilinipasa nisifiwe na ninyi; kwa sababu sikuwa duni ya mitume walio wakuu kwa lolote, nijapokuwa si kitu.

²⁰ Ningetaka, kama tu ningeweza kuliita hili somo... Na—nafikiri Roho Mtakatifu yuko miongoni mwetu. Na, sisi, isingekuwa tu ni kusoma Maandiko. Yeye, hayo ndiyo

anayoishia. Na kila Neno limetolewa kwa uvuvio, nalo linafaa kwa wakati wake. Haliishi kamwe. Ni kama mnyororo. Yanaendelea tu kusonga mbele. Hayaishi, Maandiko.

²¹ Nami niliwazia, wakati nikisoma hili, na kuwazia juu ya mahali hapa padogo, nilikumbuka jambo hili, Paulo akisema, “Nimekuwa mpumbavu.” Mnaona? Sasa, hilo ni jambo la kigeni sana kwa mtume kusema. “Nimekuwa mpumbavu.” Sasa, mpumbavu ni mtu ambaye kweli hawana akili timamu. Basi mtume huyu angeweza kusema jambo kama hili, “Nimekuwa mpumbavu”?

²² Ndipo basi kuwazia juu—juu ya kundi hili, hapana shaka, kwamba, machoni pa watu ng’ambo ya pili, wewe umekuwa mpumbavu. Umekuwa kile ambacho tungekiita, leo hii: *Wa Kipekee*. Hapana shaka watu wanakuwazia hivyo. Pia kumbuka, kwamba, ng’ambo ya pili, hao nao ni wa kipekee, pia. Unaona?

²³ Kwa hiyo—kwa hiyo huna budi kuwa mpumbavu wa mtu fulani, kwa hiyo afadhali niwe mpumbavu wa Kristo. Mnaona? Ningekuwa ninii... Mungu alisema watu Wake walikuwa “watu waliotengwa, wa kipekee; waliochaguliwa, walioteuliwa; ukuhani wa kifalme, wakitoa dhahihu za kiroho kwa Mungu, yaani, matunda ya midomo yetu, ikilisifu Jina Lake.”

²⁴ Wakati fulani uliopita... Maskini ucheshi huu, natumaini hautatatiza roho mzuri aliye humu ndani. Ndio kwanza nikumbuke. Ilikuwa ni Ndugu Troy wa Wafanya Biashara wa Full Gospel, ndiye aliyekuwa akisimulia hili. Nilikuwa nikiwazia hili, kwa ajili ya huyu kijana mwimbaji hapa, ambaye ndio kwanza amjie Bwana. Wakati a—alipokuwa akifanya kazi katika...

²⁵ Yeye ni mkata nyama, naye alikuwa anafanya kazi katika duka la nyama. Na—na huyu alikuwa ni Mjerumani pale, naye aliendelea tu kuzungumza naye juu ya Bwana. Naye huyu Mjerumani asingeweza kuzungumza Kiingereza vizuri sana. Kwa hiyo a—akasema, “Vema, njoo mkutanoni.” Kasema, “Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

²⁶ Kwa hiyo mzee huyu Mholanzi anataka ajue kwamba yeye alikuwa ni Mlutheri, mnaona, alikuwa—alikuwa ni sawa. Alikuwa ninii...?...

“Vema, wewe njoo ukatutembelee mara moja.”

²⁷ Ndipo wakakutana na ku—kundi la, labda, watu wa kipekee, pia, kama tunavyowaita. Mnaona? Basi usiku huo huyu Mjerumani akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na siku iliyofuata alikuwa akikata nyama, na kunena kwa lugha na kuimba. Alikuwa na yubile ya kawaida.

²⁸ Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, bosi wa kiwanda hicho akaja huko, na akasema, “Henry,” kasema, “kwani una nini?”

Akasema, “Ee utukufu kwa Mungu.” Akasema, “Ni—niliokoka.”

²⁹ Naye akasema, “Mbona,” akasema, “kwani umekuwa wapi?” Kasema, “Hapana shaka ulikuwa kule chini pamoja na lile kundi la nati,” akasema.

³⁰ Akasema, “Naam, utukufu kwa Mungu!” Akasema, “Ni—nilikuwa huko chini na kundi la nati.” Akasema, “Mwajua, usipokuwa na na—na—nati. . .” Kasema, “Ukichukua motokaa kwa mfano, inayosafiri barabarani. Nawe utoe nati zote kutoka kwayo, una, huna kitu ila lundo la vikorokoro!” Hiyo karibu ni kweli tu, nawe ukitoa na—na—nati kutoka kwenye chochote. Sasa, inahitaji hizo kushikilia kitu hicho pamoja.

³¹ Ulimwengu unafikia mahali fulani, katika machafuko, nalo kanisa linazama katika mambo ya kilimwengu na—na umadhehebu, na kadhalika, mpaka wakati mwingine inahitaji nati kushikilia kitu hicho pamoja. Hiyo ni kweli. Wasipokuwa nazo, tusipokuwa nazo, hatuna kanisa.

³² Sasa, tunaweza kuliwazia somo hilo kwa muda kidogo tu. Paulo alisema, “Nimekuwa mpumbavu, ama na—na—nati, kwa ajili tu. . .” Sasa, huna budi kuwa nati ya mtu fulani. Ama unaweza kuwa nati ya ulimwengu, au nati ya Kristo.

³³ Siku moja huko California, nilikuwa nikitembea mtaani, na kulikuwako na mtu fulani. Alikuwa na maandishi mbele yake, namna *hii*, yaliyosema, “Mimi ni mpumbavu wa Kristo.” Na mgongoni mwake alikuwa na maandishi yaliyosema, “Sasa, wewe ni mpumbavu wa nani?” Mnaona? Kwa hiyo, tukamwuliza, kuyahusu. Kasema, “Huna budi kuwa mpumbavu wa mtu fulani.”

³⁴ Kwa hiyo Paulo, hapa, alikuwa amechagua kuwa mpumbavu kwa ajili ya Kristo. Nanyi mnaweza kuwazia jinsi ulimwengu ulivyomwazia wakati huo; wala si ulimwengu pekee, bali kanisa. Mtu huyo alikuwa amefunzwa kuwa kuhani. Alifunzwa chini ya Gamalieli, mashuhuri, mmoja wa wasomi mashuhuri kuliko wote na waalimu mashuhuri kuliko wote wa siku hiyo. Basi wakati alipopata, labda, tuseme, Shahada yake ya Kwanza na digrii ya—yake ya Udaktari na falsafa, na—na alikuwa tayari ku—kuteuliwa kwenye ukuhani, na labda siku moja pakiwapo na uwezekano, kwa shauku aliyokuwa nayo huyu kijana mwanamume. Halafu kubadilisha hayo, mara moja, yote kwa sababu jambo fulani lilitukia. Yeye alikutana na Kristo njiani akienda Dameski.

³⁵ Halafu basi, kwa ulimwengu yeye alikuwa ni mpumbavu, na kwa kanisa alikuwa ni mpumbavu. Kwa—kwa kanisa la kimadhehebu kweli alikuwa ni mpumbavu. Hayo ndiyo aliyosema hapa, alikuwa amefanyika mpumbavu. Yeye ni mpumbavu kwa watu hao, bali alikuwa ndiye chombo ambacho Mungu alitumia, kulishikilia Kanisa pamoja, kuushikilia Mwili,

kama ulivyokuwa siku ile, pamoja. Yeye alikuwa amefanyika mpumbavu kwa—kwa ajili ya huo.

³⁶ Tunaweza kumwazia Nuhu, kama vile ndugu alivyoimba juu yake hapa, “Wakati Mungu alipoutuma upendo Wake juu ya mbawa za hua,” mmoja wa nyimbo ninazozipenda sana. Nami daima nimetamani kupata mtu ambaye angeweza kuuimba huo. Nilitaka kuuzungumzia huo.

³⁷ Siku moja nilisoma hadithi ya askari waliozingirwa, naye adui, Wajerumani katika Vita vya kwanza vya Dunia, walikuwa wamewazingira. Nao walikuwa na ma—maskini njiwa wa kupeleka ujumbe. Ndipo wakati. . . Huyu ni mfano wa hua, bila shaka. Ni mmoja wa jamii ya hua. Basi walipouweka ujumbe huo kwenye maskini njiwa huyo, aliruka juu hewani. Nazo risasi zikimlenga, kwa kila njia, maana walijua ilikuwa ni kitu gani. Ikauvunja mguu wake. Maskini miguu yake ikining’inia chini, amelemazwa. Nayo mabawa yake yalikuwa yametolewa manyoya kwa risasi. Alikuwa ameinama upande, na kadhalika, kupitia hewani. Bali akaanguka papo hapo kambini alipopaswa kufikia, nao wakapata usaidizi.

³⁸ Mnajua ninalomaanisha, tangu hapo na kuendelea. Mnaona? Kwa hiyo, tulikuwa katika hali kama hiyo siku moja, pia, mwajua. Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu na kuchubuliwa kwa maovu yetu, bali ujumbe ulifika hapa, hata hivyo. Alituletea ujumbe.

³⁹ Nuhu, katika siku zake. Ninaweza kuwazia mtu wa wadhifa wake, nabii aliyethibitishwa na Mungu. Na—na Mungu alinena naye siku moja. Lilikuwa ni jambo la kigeni jinsi gani, katika wakati mkuu wa kisayansi. Labda wangeweza kurusha kwenye mwezi kwa rada yao, nao wangeweza kujenga sfinksi na piramidi. Ndipo—ndipo Mungu akanena naye na kusema, “Nuhu, maji yatanyesha kutoka mbinguni.” Ungeweza kuwazia mtu wa wadhifa wake, nabii wa Bwana, akitoka kwenda na ujumbe wa kipumbavu kama huo, na kusema hivyo?

⁴⁰ Kamwe haikuwa imenyesha, kumbukeni, kutoka mbinguni, katika siku hizo. Mungu alitia nchi maji, Biblia inasema, kwa umwagiliaji kwa mitaro na kadhalika, chemchemi. Haikuwa imenyesha hata tone moja. Hapakuwapo na maji huko juu. Kwa hiyo wangeweza kuthibitisha hakukuwa na maji huko juu.

⁴¹ Ndipo mtu akatokea na ujumbe. Wala si hayo tu, bali akajitenga na walimwengu wengine. Akawa nati kwa ulimwengu. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ni nati ya wakati wake. Jinsi ambavyo mtu aliye na ujumbe wa kiwazimu kama huo, angejaribu kuwatoa watu nje kwa maskini trela ndogo, ama safina, ama chochote kile wa—walichokuwa wakijenga huko juu. Naye—naye alikuwa—kweli alikuwa mtu mpumbavu.

⁴² Lakini alifanya nini? Katika kufanya hivyo, yeye alikuwa ndiye nati iliyoliokoa Kanisa lililoamini katika siku hiyo. Naam,

bwana. Hayo ndiyo yaliyotendeka. Ilibidi awatoe kutoka kwa ulimwengu. Lakini alikuwa akiandaa mahali ambapo alijua ya kwamba Kristo angekuja na kuwachukua. Yeye akawa nati.

⁴³ Ninyi, mngeweza kumwazia Musa katika siku yake, mtu akishuka kwenda kwa mwenye akili sana? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Waliushinda ulimwengu wakati huo. Na mambo yao ya kisayansi na ninii yao—sanaa yao na kadhalika, kweli, nadhani, yalishinda yetu leo hii. Na uhodari wao wa sanaa na wa ujenzi, na kadhalika, na mambo makuu waliyofanya wakati huo, katika—katika siku hiyo.

⁴⁴ Basi ungeweza kuwazia mtu akishuka kuja pale, na kusema alikutana na—na—na Mungu ambaye hata hawakumwamini, katika kichaka kilichowaka moto? Naye akashuka... Akiwa ni mwanajeshi, kwanza, naye alikuwa amefunzwa katika ujanja wote wa—wa—wa ulimwengu wa kijeshi. Nasi tunaona ya kwamba anashuka kuja kule na kijiti mkononi mwake kuwachukua na kuwakomboa watu kutoka kwa taifa lililo—lililouteka ulimwengu.

⁴⁵ Mbona, kwa Farao, yeye alikuwa ni nati. Hivyo tu. “Alikuwa mwendawazimu.” Kasema, “Hebu ajaribu, aendele, apayuke. Atajitangaza kwamba ni mwendawazimu.” Vema, sasa, kwa Farao kweli, na ulimwengu wake mkuu wa kisayansi, alikuwa ni wa kipekee. Alikuwa ni nati kwa—kwao. Mnaona? Alikuwa nati.

⁴⁶ Lakini alifanya nini? Aliwakomboa watu hao, kwa maana alitumwa na Mungu. Ilihitaji... Inahitaji kitu kisicho cha kawaida, kitu ambacho ni tofauti na ulimwengu mwingine wote. Mnaona, ulimwengu uko upande mmoja sana kwenye ninii kuu... mafanikio yao makuu ya kisayansi, na kadhalika. Na wakati mtu anapoongozwa na Mungu, kufanya kitu ambacho si cha kawaida, anakuwa mpumbavu. “Yeye ni mwendawazimu.” Lakini, mnaona, inahitaji kitu kama hicho, kushikilia kitu hicho pamoja.

⁴⁷ Sasa, tunawazia juu ya Eliya katika siku zake. Wakati, Ahabu na Israeli, wakati huo, waliogopewa na kila taifa chini ya mbingu chini ya utawala wa Ahabu huyu. Naye Ahabu alikuwa ni mtu mashuhuri. Ilikuwa ni siku kuu, kitu kama jinsi tulivyo sasa. Kanisa lilikuwa lote limekuwa la kimtindo. Mnaona? Ilikuwa ni kujipodoa kwa Yezebeli, na—na upotovu wa Ahabu, na kupatana, nao walikuwa wameyabomoa madhabahu ya Mungu. “Loo, ukiitumikia miungu tu, inaleta tofauti gani? Mnaona? Tutapanda twende kwenye vijisitu, nanyi mnaweza kumtumikia mungu yeyote mtakaye.”

⁴⁸ Hivyo ni kama tu jinsi ilivyo leo, mnaona, mitindo yote, na—na—na mavazi, na nguo, na mambo ya ulimwengu. Na, “Loo, kama ukitaka kuwa mfuasi wa *hili*, uwe mfuasi wa *lile*, uwe mfuasi wa *hili*, uwe mfuasi wa *lile*, ni sawa. Mnaona? Mradi tu unahudhuria kanisa, haileti tofauti yoyote.”

⁴⁹ Inaleta tofauti, kile—kile ninachofuata, na ni Mungu gani ninayemtumikia, na jinsi ninavyomtumikia. Anayo njia moja ya mimi kumtumikia, Yeye ameliandika hilo katika Neno hili. Na hivyo ndivyo itupasavyo kumtumikia. Mnaona? Sasa, inaleta tofauti.

⁵⁰ Lakini wakati Eliya alipokuja huko nje na Ujumbe kama huo aliokuwa nao, mngeweza kuwazia? Yeye akawa nati kwa—kwa—kwa Farao, ama kwa... Samahani. Kwa Ahabu, akawa nanii wa kawaida... Kujitenga! Lakini, mnaona, kulikuwako na elfu saba miongoni mwa watu hao, mnaona, wangaliweza kuokolewa. Mnaona? Naye akawajia. Ilimbidi kuwa nati kwa ulimwengu, kusudi awapate. Vivyo hivyo na Nuhu, ilibidi awe nati kwa ulimwengu apate kuwapata watu wanane, pamoja naye mwenyewe. Mnaona? Ilibidi awe mtu wa—wa kipekee.

⁵¹ Amosi, katika siku ambazo aliuleta ujumbe wake, naye akatabiri. Nasi tunaona, ya kwamba, wakati alipokuja Sa—Sa—Samaria, ambao ulikuwa umejitolea kwa ulimwengu. Nao wanawake mitaani walikuwa karibu wamekuwa ukahaba wa umma. Nayo mitindo, ilikuwa ni Hollywood ya kisasa. Wakati maskini jamaa huyu mdogo mwenye kipara, asiyejulikana alipoinuka, juu ya mlima asubuhi moja, na kuangalia chini Samaria, na kuuona katika dhambi, na, mbona, ningewazia moyo wake nusura uzimie.

⁵² Jambo pekee alilokuwa amejua, yeye alikuwa mchungaji. Kweli hakuwa... Bwana alimpa tu ujumbe huu na kumtuma kule chini. Na sasa hakuwa na udhamini. Hakuwa—hakuwa na mtu wa kumuunga mkono. Bali aliongozwa na Mungu kwenda, kuuleta ujumbe huu kwa watu, na kuwaita watoke kwenye hukumu.

⁵³ Vema, sasa, ningewazia, kwa wakati mkuu wa kisayansi na wakati wa anasa, kitu kama ilivyo leo hii, Amosi akawa wa—wa—wa kipekee. Mnaona? Akawa mpumbavu, nao—nao wasingetaka uhusiano wowote. Lakini, hata hivyo, yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Naye akakomboa walioweza kukomboleka.

⁵⁴ Yohana Mbatizaji, alipokuja katika siku zake, ule ulimwengu mkuu wa kidini, akitoka, katika, kutoka kwenye nyika kama hili, kutoka kwenye miamba na kadhalika kwenye nyi—nyika ya Judea. Wala hakuvikwa kama kuhani. A—alivaa nguo mbovu za mfanyakazi, labda, akiwa amejizungushia va—vazi, sio mwalimu mkuu wa seminari ya kitheolojia ama ninii, kadhalika. Lakini a—alikuwa ni mtu wa kawaida tu ambaye angeweza kufanya kazi kwa mikono yake, ama chochote kile. Wakati aliponinii—wakati aliposhuka kuja, kutoka nyi—nyikani kule, amejizungushia ngozi ya kondoo, alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, kwa kuwa alijua ya kwamba wakati wa Masihi ulikuwa ni huo.

55 Yeye angeweza kujitambulisha kabisa katika Neno la Mungu. Alisema, kwa kuwa kumbukeni, alijitambulisha mwenyewe katika Malaki mlango wa 3, mnaona, kama mjumbe wa kukutangulia kuja kwa Bwana. Alijua kule kuja kulikuwa karibu sana mpaka ilibidi a—ajitokeze. Vema, watu walidhani alikuwa ni mtu mshenzi, m—m—m—mpumbavu tu. Mnaona?

56 “Nati,” tungeita siku hizi. Sababu ya mimi kuchagua neno hilo “nati,” halivutii. Lakini, hata hivyo, hilo, ni neno zuri kwa yale ninayotaka kulitumia kwayo, kwa sababu huo ndio msamiati wa mitaani ungeninii, utalitumia leo hii. “Ni nati tu ya—ya kawaida,” tungemwita.

57 Vema, huyu hapa Yohana Mbatizaji. Yeye anakaa tu kule nyikani, akihubiri mahubiri yake madogo, huku na huku kule, katika—katika Yordani, akitembea huku na huku kwenye huo ufuko wa mto, akilia, “Wa—wakati umewadia! Basi tokeni mkajitenge. Masihi yuaja!” Mbona, ningewazia makuhani na hao wote, alikuwa tu amekuwa nati wa kawaida. Hivyo tu. Mnaona, hivyo ndivyo tu alivyokuwa, wa kipekee tu. Na hao waliomfuata wakawa wa kipekee, kwa ufupi ni wapumbavu tu.

58 Mnajua Bwana wetu alitangazwa kuwa kitu hicho hicho hapo alipokuja, mwendawazimu? Mnaona? Yeye hakuvingia kule mijini na—na kwenye mashirika yao makuu, wala—wala kujiunga nayo, na kadhalika. Alikuwa akiwaita watu. Alikuwa akiwaita watoke. Naye alihesabiwa, na wanadini, siku Zake, nati ya kawaida.

59 Kama tu vile Paulo alivyokuwa katika siku zake, mtu aliyefunzwa, na hata hivyo ange—angefanya jambo kama hilo alilofanya, kujitenga na ulimwengu mwingine, na madhehebu, na—na kujaribu kuwaita watu. Alikuwa ni mtume kwa kanisa la Kimataifa. Yeye ni mtume wetu, tu—tunajua hilo, kwa kanisa la Kimataifa. Alikuwa nati iliyolitoa kanisa la Mataifa kutoka kwa ukafiri wa Kirumi, na ibada za kipagani za siku hiyo.

60 Martin Luther, alikuwa nati kwa kanisa Katoliki. Mnaona? Ungeweza kuwazia kuhani a—aliyekuwa ametupilia ninii yake, mafundisho yake yote, mbali, ya kanisa, na kukataa kutoa ushirika huu kwa sababu kanisa lilisema, “Ni mwili wa Kristo”? Naye alijua alikuwa... wa—watawa na kadhalika walikuwa wameutengeneza mkate huo mwembamba huko ndani. A—alijua hicho hakikuwa Kristo. Hicho kilikuwa ni kipande cha mkate, mnaona, mkate mwembamba wenye sukari. Naye alijua ya kwamba, ya kwamba hiyo divai haikuwa Damu halisi ya Kristo. Iliwakilisha tu. Kwa hiyo, a—a—aliitupa chini, katika—katika ninii yake—imani yake nyofu, wala hakutaka uhusiano wowote nayo. Unaona? A—a—alimalizana nayo.

61 Sasa, labda, kanisa Katoliki lilisema, “Loo, achaneni naye. Angalieni ni kundi do—dogo jinsi gani alilo nalo huko nje. Yeye ni kitu gani? Yeye ana ya ba—bandia tu. Nasi, kanisa kubwa.

Hivyo tu. Ni kitu tu.” Lakini, mnaona, yeye alikuwa ndiye nati, mnaona, iliyokuwa ikilishikilia pamoja, mnaona, katika yale matengenezo. Alileta matengenezo.

⁶² Vipi kuhusu wakati alipojiundia dhehebu na kufikia mahali... Na—na baada ya kifo chake, na ule—ule ujumbe aliokuwa amehubri kwisha, basi kanisa likawa baridi na gumu tena, hata Mungu akainua nati nyingine, a-ha, iliyoitwa John Wesley. Hiyo ni kweli. Vema, yeye alikuwa ni nati kwa kanisa la Kianglikana. Mnaona? Lakini alifanya nini? A—aliuokoa ulimwengu, ulimwengu, Kanisa lililokuwa ulimwenguni, naomba kusema. Aliliokoa Kanisa lililokuwa ulimwenguni. Kwa nini? Kwa kufanyika nati. Hiyo ni kweli. Aliokoa.

⁶³ Nini basi? Na sasa, basi, tunakuja moja kwa moja baada ya wakati wake, nao ule wakati mkuu wa Kiwesley ukapita, ndipo tukawa na Wabaptisti kutokana na John Smith, ndipo wakawa na Alexander Campbell, na—na halafu tukawa na Buddy Robinson wa Nazarayo. Na hatimaye ikaendelea kupeperuka, mbali na mzunguko halisi.

⁶⁴ Ndipo Mungu akainua kundi lingine la nati: Pentekoste. Nao wakawa nati kwa watu. Hao ni wendawazimu, kwa ulimwengu. Lakini walifanya nini? Walifanya kazi kuu. Hakika walifanya, ule wakati wa Kipentekoste.

⁶⁵ Sasa, sasa, ninaamini wakati umewadia wa kuinuka kwa nati nyingine. Na hivi hamwazii hivyo? Na—nafikiri ni karibu tu... Pentekoste imefanya jambo lile lile ambalo—ambalo ulimwengu mwingine uliingia. Lakini wakati umewadia kwa ajili ya nati nyingine. Mnaona? Kwa hiyo kama inatubidi kuvuta kando kidogo, kwenye upande *huu* wa ufuko, mnaona ninachomaanisha? Nao watu wanadhani sisi ni wa kipekee sana na wasio wa kawaida, jinsi tunavyojitenga, jinsi tumefanya hapa. Nasi hatu—hatujatengana. Sisi ni kitu kimoja. Mnaona? Mnaona? Jinsi tulivyo, tulijitenga na ulimwengu.

⁶⁶ Ndugu Leo, aliongozwa kuja hapa, na hapo mlikuwa na watoto wadogo wanaopaswa kufunzwa. Mnaona? Mnao wanawake, wasichana hapa, ambao—ambao hawapendi kuenenda kwa jinsi ya ulimwengu. Mna wanaume hapa, ambao ni wazee na wanastaafu. Wanataka mahali ambapo wanaweza kutulia na kujisikia nyumbani. Mnaishi miongoni mwa watu wa aina yenu wenyewe. Vema, na, mnaona, nafikiri Mungu anaweza kuinua kitu fulani cha kushughulikia hayo. Hivi hamwazii hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni—ninaamini hilo kwa moyo wangu wote, kwamba Yeye hufanya hivyo.

⁶⁷ Sasa, tunaona, wakati umewadia sasa. Angalieni, nati daima ndiyo iliyowavuta pamoja.

⁶⁸ Kama vile Wamarekani wote leo hii, tunaona ulimwengu mwingi sana na kadhalika, katika makanisa yetu na madhehebu yetu, na kadhalika. Hebu jambo fulani liinuke kwenye Neno.

Mnaona, wanaelekea kwenye kanuni hiyo ya imani wala si kwa Neno. Na hebu kitu fulani kiinuke pamoja na Neno, mwajua.

⁶⁹ Mnasema, “Vema, watu wanafikiri mlijitenga wenyewe.” Nilizungumza na mchungaji wenu hapa, na Ndugu yetu Leo. Ndipo mtu fulani akasema, “Vema, mbona usije, na uingie kwenye *hili*, na uingie kwenye *lile*?”

⁷⁰ Yeye alisema, “La, la.” Unaona, yeye amejitolea mhanga kwa kitu kimoja, Neno, mnaona, kwa Neno. Mnaona?

⁷¹ Vema, sasa angalieni. Kama kuna nati iliyotumwa, hapana budi pawe na bolti itakayotoshea. Hiyo ni kweli? Sasa, Mungu huzituma nati. Hivi hamwamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Nitalielezea hili katika kitambo kidogo. Lakini kulifafanua. Hapana budi pawe na bolti, nayo bolti hiyo haina budi kutiwa hesi, ipate kuingiana na nati.

⁷² Nina furaha sana kutiwa hesi na Neno. Nina furaha kwamba kuna bolti iliyotiwa hesi vivyo hivyo. Nayo inapaswa kufanya nini? Ni kuvuta Bibi-arusi kutoka ulimwenguni, kumweka kando kwa ajili ya jambo la tofauti. Naam, enyi marafiki. Huenda tukawa nati kwa mambo ya ulimwengu, watu wa ulimwengu, bali tunavuta nje tu, kile ambacho kimetiwa hesi kwa ajili ya hii.

⁷³ Nuhu alikuwa ametiwa hesi katika siku zake, na hao manabii wengine, na kote katika wakati. Nao watu wenye haki walitiwa hesi, kwa sababu Yeye aliituma. Ingekuwa na faida gani kuwa na bolti ama nati, kama huna bolti ambamo itaingia? Nayo bolti na nati, pamoja, zafaa kufanya nini? Ni kuvuta kitu pamoja. Mnaona? Nao ni uweza wa Kristo wa kuvuta, ambao hutuvuta kuttoa kwenye mambo ya ulimwengu. Mnaona? Ndipo tunashiriki na huduma kuu ya Paulo, tukisema, “Nimekuwa mpumbavu.” Kwa hiyo watu wanapofikiri wewe ni wa kipekee, unaona, unaona mahali unaposimama? Unaona? Umekuwa mpumbavu kwao, upate kuvutwa na uweza wa Mungu. Ambao kwao, kitu Fulani ndani yako, kitu Fulani moyoni mwako kinakutia hesi.

⁷⁴ Huenda nikasema asubuhi ya leo, “Ni nani Methodisti, Mbaptisti, Mpentekoste Assemblies, *hili*, *lile*, na *jingine*?” Kungekuwako na kila namna ya mikono itakayoinuliwa hapa, na watu arobaini, hamsini. Mnaona? Kungekuwako na wengi hivyo, kila mtu ni tofauti.

⁷⁵ Lakini ni kitu gani kinachowafanya kuketi hapa? Kwa nini mpo hapa. Mnaona? Ni kwa sababu ulitiwa hesi kushikana na kitu fulani. Mnaona? Na kinapoanza kuja, kinafahamika kwako. Ukijaribu kuweka hesi fulani katika bolti, namna fulani ambayo isingetoshelea, haileti maana kwako. Mnaona, ha—haitaendelea. Mnaona? Lakini kitu fulani kikija ambacho kinaenea vizuri kabisa, kinakuvuta kutoka Chikago, kutoka New Orleans, na popote unapotoka, kuja hapa. Mnaona? Na sasa, mnaona,

unakuwa wa kipekee, hakika kabisa, kwa ulimwengu. Bali usiache hilo likusumbue. Unaona? Usiache hilo likusumbue.

⁷⁶ Sasa unasema, “Nitajua je kwamba nimetiwa hesi vizuri?” Liangalie Neno. Unaona? Sasa unajua kama umetiwa hesi vizuri, kama sisi ni nati za Kristo, ama kama sisi ni nati kwa ulimwengu.

Sasa ulimwengu, pia, umepokea nati ya—yao. Kweli kabisa.

⁷⁷ Nilikuwa na kitu kidogo kilichoandikwa hapa, nilitaka, sikutaka kukisahau. Ni—ninii. . . Nasi tunaketi hapa, tunakuwa bolti, nati kwa ulimwengu, hiyo ni kweli kabisa, tupate kuushikamanisha Ufalme wa Mungu pamoja, duniani; mnaona, Ufalme wa Mungu, pamoja. Vema.

⁷⁸ Kumbukeni, ulimwengu, wao—wao, ulimwengu wa nje, wana nati zao pia. Shetani huwapa nati, katika siku za kitu hiki kikuu. Mnaona, yote inatenda kazi, upande mzuri na mbaya. Mnaona? Sasa katika siku za . . .

⁷⁹ Ulimwengu ulikuwa na nati, na hiyo ilikuwa ni Farao, katika siku za—za Musa. Kulikuwako, mnaona, ilibidi kuweko. I—ibilisi ana nati zake pia. Vema, kulikuwako na Farao. Mnaona? Sasa, Israeli; naye Musa akisimama kule chini, alikuwa awavute hao watu watoke, alikuwa ni nati kwa Farao. Lakini Farao pia alikuwa ni nati kwao, pia. Mnaona?

⁸⁰ Na kwa hiyo inabidi iwe hivyo. Kwa hiyo, wewe ni nati ya mtu fulani. Nina furaha sana kuunganishwa katika Neno, nanyi je, kwa—kwa hesi ya Hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mtu fulani atafundisha Hilo.

⁸¹ Ahabu, yeye alikuwa ni nati, hakika, kwa Eliya na wale elfu saba, kundi lake lote kule nje. Yezebeli katika madoido yao yote na kadhalika waliyokuwa nayo huko nje, ambaye alikuwa ni nati kwa hao elfu saba, wasiompigia Baali goti lao. Na vivyo hivyo Eliya alikuwa nati kwao, mnaona, jambo lile lile.

⁸² Tunaona, katika siku za Herode, Yohana alikuwa ni nati. Mnaona? Naye Herode alikuwa ni nati pia. Ulimwengu ulikuwa na moja. Vema.

⁸³ Katika siku za Yesu, Yeye alikuwa m—m—m—mpumbavu kwa—kwa ulimwengu, mnaona, kwa Pilato. Lakini Pilato alikuwa nati, pia, ya kumkataa. Hiyo ni kweli. Mnaona? Yeye hakuwa ametiwa hesi. Alikuwa na nafasi. Bali wakati alipopata nafasi yake ya kulikubali, yeye alitaka namna fulani ya mchekeshaji, namna fulani ya ujanja, namna fulani ya sungura wa kichawi anayetolewa kwenye kofia, mwajua, ama kitu fulani. Yeye alisema, “Loo, ningetaka kukuona ukifanya ujanja fulani,” mwajua, ama kitu kama hicho. Alikuwa ni nati, yeye mwenyewe. Mnaona? Alikuwa na nafasi ya kulipokea, bali hakulipokea.

⁸⁴ Masadukayo pia, na Mafarisayo, walikuwa ni kitu kile kile siku hiyo, kwa kutomkubali Paulo, yule aliyesema alikuwa mpumbavu kwa ulimwengu. Mnaona?

⁸⁵ Lakini kanisa lina nati zake, pia. Mnaona? Nao ulimwengu una nati zake. Kristo ana Zake. Mnaona? Sasa wewe ni wa nani? Njia pekee unayoweza kujua. . .

Unasema, “Ninajua je kwamba hili ni kweli, Ndugu Branham?”

⁸⁶ “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa hiyo, Neno lingali ni Yeye. Kwa hiyo kama tumetiwa hesi na Hilo, mnaona. Kujua, sisi, ingawa sisi ni nati kwa u—ulimwengu, kama tumetiwa hesi katika Neno la Kristo, Naye Kristo analionyesha, ambapo Yeye—Yeye analivuta pamoja, mnaona, kulivuta Kanisa Lake pamoja. Acha wainuke na wafanye watakalo.

⁸⁷ Sasa, Yesu, katika Mathayo 24:24, alisema kwamba, “Makundi haya mawili yangefanana sana, katika siku za mwisho, kuwadanganya walio wateule, kama yamkini.” Watu, bado, watu wakati fulani katika Pentekoste, kwenu mliotoka nje ya Pentekoste, mnaona. Wanapounda dhehebu na kwenda kule katika makundi kama hayo, nanyi mnatoka kwake. Mnaona, Biblia ilisema, kwamba, “Ingewadanganya walio wateule kama yamkini.” Mnaona? “Walio wateule,” hao ni wale walioteuliwa kufanya jambo hili; hao, mnaona, hiyo bolti.

⁸⁸ Usije, ukasema, “Loo, yao pale, kuna nati, unaona.” Unaona, hana budi kuwa, amefikia ambapo ninii. . . Wakati hesi zinapokatwa katika bolti, nati inapaswa kukatwa vile vile. Mnaona ninachomaanisha? Haina budi kuenea. Mnaona? Nao Wateule, basi, mnaona, haitakazwa na kitu kingine chochote. Inapaswa tu kuja kwa Kristo. Mnaona? Ndicho kitu pekee kitakachoenea. Mnaona? Na hapo ndipo tunaposimama leo hii. Shukrani ziwe kwa—kwa Mungu. Na sawa.

⁸⁹ Sasa, tunaona, pia, ya kwamba u—ulimwengu una nati yao. Nanyi mwajua, kuna mengi sana yangeweza kusemwa. Hatuna wakati wa kuyasema, bila shaka. Lakini, hili, wazo hili moja, kwenu.

⁹⁰ Ninaliona maskini kundi hili zuri la kina mama walioimba pale, dakika chache zilizopita. Jamani, laiti ningalikuwa na wimbo huo. Ninasieni huo kwa kanda, sivyo, nyimbo hizi? Wakati nyote mnapoimba hapa, mkitunga wimbo wakati mmoja. Nitawalipa kwa kanda hiyo. Mnaona? Ningetaka kuwa nayo. Mnaona? Hiyo ilikuwa nzuri sana, hiyo ibada tamu halisi namna hiyo.

⁹¹ Sasa, mwajua, kulikuwako na ninii—ninii. . . Vijana, wanawake wa siku hizi, hao, Wakri-. . . wanaojiita Wakristo,

wanawake ambao—ambao wanaenda kanisani, wa—walitaka kitu fulani cha ku—ku—kuwaridhisha. Walijua ya kwamba ha—hawakuwa wakikipata, ni kwenda kanisani tu. Bali wanataka kudumisha ushuhuda wao vivyo hivyo. Mnaona? Walitaka kuushikilia ushuhuda wao, “Mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti. Mimi ni Mkristo, mnaona.” Walitaka kuvua nguo zao. Walitaka kuvaa kaptura na bikini, ama vyovyote mnavyoyaita, na yote wangiweza kuona. Hao, hao walitaka kufanya mambo haya. Walitaka kukata nywele kama wanaume, na—na—na kufanya mambo haya.

⁹² Na kwa hiyo wa—walitaka kufanya hivyo. Mnaona? Na, hata hivyo, hivi mlipata kuwazia ni kwa nini walifanya hivyo? Yesu alisema, “Roho hizo mbili zitafanana sana, ingewadanganya walio Wateule.” Hilo halina budi kutimia. Mnaona? Mnaona? Kwa hiyo, walitaka kufanya hivyo. Hawakupata . . .

⁹³ Mwa—mwanadamu hana budi kuabudu. Huna budi kuabudu kitu fulani. Wewe, liko tu ndani yako, kuabudu. Kwa hiyo mwanadamu hana budi kuabudu kitu fulani. Kwa hiyo, hawakuwa na ibada yoyote katika kanisa lao, kwa hiyo Mungu akawainulia nati, Elvis Presley, Pat Boone. Wangali wanaushikilia ushuhuda wao. Elvis Presley, Mpentekoste. Pat Boone, wa church of Christ. Mnaona, nati kabisa kuyatimiza Maneno ya Yesu hapa, “Wangefanana sana, ingewadanganya walio wateule, kama yamkini.” Wangali wanashikilia, wanaimba nyimbo Jumapili, na roki Jumatatu. Mnaona? Kwetu sisi, hiyo—hiyo ni nati. Mnaona? Kweli, ndivyo ilivyo.

⁹⁴ Sasa, lakini, mnaona, mle ndani Yeye alikuwa na wanawake wazuri, pia, waliotaka kutenda kama mama wa heshima. Walikuwa na mwenendo mwema ndani yao. Walitaka kuwa kile Kristo anawataka wawe. Kwa hiyo anamtuma mtu na ujumbe, ambao—ambao kwa kanisa wanaloshiriki ni upumbavu, yeye anakuwa nati. Lakini mnaona, jambo ni kwamba, inaenea vizuri kabisa. Unaponena juu ya nywele ndefu, na kuonekana kama mama wa heshima, na kuvalia kama mama wa heshima, na kutenda kama mama wa heshima . . . Badala ya kusimama hapa kama wasichana hawa asubuhi ya leo . . .

⁹⁵ Nilikuwa nikimwangalia msichana mdogo pale, macho yake yalionekana ya Kimbinguni. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . kama kioo, wakati alipoangalia juu namna *hiyo*, akiimba, kitu fulani moyoni mwake. Waangalieni hapa, wakati hao wasichana walipoimba. Nikawazia, “Ee Mungu! Vema, vipi kama—kama nyota wa Hollywood ange—angepata hicho moyoni mwao? Wangukuwa kitu kile kile.” Mnaona? Lakini ni nini? Kwa nini wakapita njia *ile*? Usingeweza kumvuta mmoja wa hao wasichana katika Hollywood. Kama ungalimpa dola elfu kumi kwa siku, asingeenda. Kwa nini? Yeye ametiwa hesi namna nyingine. Hiyo ni kweli kabisa. Ametiwa hesi namna nyingine. Hiyo ni kweli.

⁹⁶ Usingeweza kumvuta Leo, Gene na hao wengine uwaingize katika madhehebu fulani. Kwa nini? Wasingewavuta ninyi watu wawaingize katika moja. Kwa nini? Mmetiwa hesi namna nyingine. Mnaona? Kwa hiyo kama umetiwa hesi, hapana budi pawe na nati mahali fulani! . . .? . . . mnaona, ku—kushikilia hilo pamoja. Hiyo si ni kweli? Mnaona? Basi ni kamilifu.

⁹⁷ “Shukrani kwa Mungu,” kama maskini yule Mdachi alivyosema, “kuhusu nati. Ukizitoa, inakuwa lundo la vikorokoro.”

⁹⁸ Mna nini? Kundi la umadhehebu, kundi la utaratibu baridi, hamna Kristo ndani yake hata kidogo, hamna Neno ndani yake hata kidogo, lundo tu la kanuni za imani, na kadhalika. Nanyi mna nini? Hebu utoe nati, una lundo la vikorokoro, hiyo ni kweli, si kitu ulimwenguni ila kuni, kitu ambacho kinangojea miali ya moto na adhabu za Mungu, kuhukumu na kuchoma moto, siku moja.

⁹⁹ Kwa hiyo nina shukrani asubuhi ya leo kuenea moja kwa moja ndani, hapa juu, mnaona, ambapo huenda ukawa ni mtu wa kipekee upande huu wa mto. Hata baadhi ya watu wako huenda wakafikiri wewe ni mtu wa kipekee. Ninajua wanafikiri hivyo. Nimepata nyaraka kutoka kwao, mnaona, zilizosema ninyi ni wa kipekee, ninyi ni tofauti, “kwani mlipatwa na nini” nyinyi? Nilichagua tu jambo hili dogo kuwaambia asubuhi ya leo. Mnaona? Hakika, ninyi ni nati. Hiyo ni kweli. Lakini ninafurahi kuwa moja. Kwa kuwa kama mimi sijafungamanishwa na Neno hili, basi mimi ni “vikorokoro.” Mnaona? Nitakuwa tu nati kwa ajili ya Kristo. Naam.

¹⁰⁰ Ninapata barua kutoka kwa wengi wa watu wenu. Baadhi yao hupita hapa na kusema, “Unajua kilichotukia?”

“Ati nini?”

¹⁰¹ “Huyu jamaa wa kipekee,” a-ha, “*fulani na fulani*, alipanda kwenda kule na kufanya *fulani na fulani*.”

Nikasema, “Hebu kidogo.”

¹⁰² Inategemea umefungiwa kwenye kitu gani. Mnaona? Kwa hiyo, Bwana Yesu Kristo, Mchungaji wa kundi la kondoo, na aiweke mioyo yenu imezungushiwa Yeye, hata, hapo yule Mchungaji mkuu atakapoonekana, tutaonekana pamoja Naye.

Twaweza kuomba?

¹⁰³ Baba wa Mbinguni, nikiona kuwa wakati umekwisha, nimeharakisha tu. Kundi zuri la kupendeza sana, la Wakristo. Na somo fidhuli hivi; bali mle chumbani hivi majuzi, nikiwazia yale niliyoona kwenye barua, na yale niliyowasikia watu wakisema. Wakati niliponinii. . . Maskini watumishi wako hapa waliniomba nije nikawatembelee, na kushiriki pamoja na kundi hili dogo. Somo hili fidhuli la kuwa nati, niliwazia nitatumia hilo, niweze kupata wa—wazo hilo kuwafikia. Wa—wangeelewa

kile ninachowazia, pia. Tumekuwa wapumbavu, kama Paulo, kwa ulimwengu. Lakini hata hivyo, Bwana, tunataka kukazwa sana Kwako na kwa Neno Lako, hata, wakati Unyakuo utakapokuja, tuta—tutapenda kuwa pamoja nao, Bwana. Kwa hiyo tusaidie daima kuiunganisha na kuifunganisha mioyo yetu katika upendo wa Kristo.

¹⁰⁴ Mbariki Ndugu Leo, Ndugu Gene, na Ndugu Daulton, na wanaume hawa wazuri na wanawake hawa wapendwa humu ndani. Kusikia shuhuda zao, wenye furaha, furaha, walioridhika. Kutembea mle chumbani, ambamo mmoja aliyepooza, na kuona hizo tabasamu! Si ajabu, Ndugu yetu Leo alisema ni mwanga mdogo wa jua, kuja hapa. Si ajabu, kuona wakati mtu, hata si wa jamii yake, si lolote ila kuhusika, hata wangechukua trela na kuifanya hivi kwamba atakuwa na furaha. Unaona, Bwana, hesi hufanya kazi sawasawa. Unaingia humo nyumbani, na kuona mtu ambaye kweli angekuwa wa kunung'unika, na—na mwenye chuki, na mwenye nia mbaya, kwa sababu kwamba—kwamba hawako huko nje na kuweza kukimbia na kucheza na—na kukata, kama wanawake wengi. Lakini yeye ana furaha kuwa hapa pamoja na wa aina yake, na kuwa hapa pamoja na Neno la Mungu, ambapo linaweza kuhubiriwa, pasipo na kanuni yoyote ya imani iliyobandikwa Mle; Neno la kweli lisiloghoshiwa la Mungu, kuabudu katika Roho. Kuja mahali padogo kama hapa, ni trela ndogo ambapo tunakutanika pamoja. Ni kanisa. “Palipo wawili ama watatu wamekutanika, niko miongoni mwao.” Tunajua Wewe upo hapa, Bwana, nasi tunakuabudu na kukusifu.

¹⁰⁵ Ninaomba, Mungu, ya kwamba utaweka ugonjwa mbali nao. Mweke adui ng'ambo ya pili ya mto. Jalia kutoka huku kuuu, huenda ikawa katika hali ndogo, lakini, Bwana, siku moja kutakua. Nami ninaomba, Bwana, ya kwamba maskini kutoka huku kudogo hapa, kwamba Wewe—Wewe utakuwa pamoja nao kama ulivyokuwa na Musa na hao wengine, wakati wakivuka Yo—Yordani, na, Yohua, wakati akienda kwenye nchi ya ahadi.

¹⁰⁶ Nami ninaomba ya kwamba utawasaidia, Bwana, na kuiweka mioyo yao iwe ya halisi, inayokuamini Wewe. Na uwabariki wakati wakilifundisha Neno. Na jalia waishi maisha marefu, ya furaha. Na siku moja, kama tukiweko huku, Bwana, tukiishi duniani wakati utakapokuja, jalia kutokee makelele kutoka upande huu wa tawi huko nje, nalo Kanisa lipae juu. Tujalie, Bwana. Kwa sababu, mtu fulani hakuwa... alikuwa mpumbavu kutosha kwa ulimwengu, kuwa nati, kuushikilia pamoja, Bwana, mpaka utakapokuja.

¹⁰⁷ Halafu, kama vile Yohana wa kale, kutoka kwenye siku zilizopita. Kama vile maskini wasichana hawa na hao wengine wanavyoimba, “Tumejitenga.” Na jinsi ambavyo ilibidi awe peke yake. Lakini, alipofanya hivyo, maskini kanisa dogo alilokuwa amelikusanya pamoja... Wakati alipomwona Yesu,

yeye alisema, “Sasa kazi yangu imekwisha. Yeye anazidi; mimi ninapungua.”

¹⁰⁸ Baba, ninaomba ya kwamba Wewe daima utatudumisha wenye furaha na wenye afya. Jalia tukutane mara nyingi zaidi, duniani, na wanaokupenda na kukutumikia. Jalia baraka Zako za Kiungu zikae juu ya ibada hii, juu ya ibada zitakazofuata. Na jalia sote tuishi hivyo katika maisha haya, katika maisha yajayo, tutakuwa na Uzima wa Milele katika ule wakati mkuu ujao, huko kwenye ule Utawala mkuu wa miaka Elfu ambako tutamwona Yeye na kuuangalia uso Wake, na kumwona. Katika Jina la Yesu, naomba. Amina.

¹⁰⁹ Mungu awabariki, enyi watu wangu. Nasikitika sana kwamba mimi, pia, ni—ni—nilichukua somo kitu kama hicho, mnaona, kitu fidhuli kama hicho. Lakini mnafahamu nilichomaanisha. Mnaona? Kwa hiyo, wakati mtu yeyote, wanasema ninyi ni wa kipekee, mnajua ni kwa nini ninyi ni wa kipekee, sivyo?

Mungu awabariki, Ndugu Leo.



WA KIPEKEE SWA64-0531
(The Oddball)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 31 Mei, 1964, kwenye Pine Lawn Trailer Park huko Prescott, Arizona, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org